**SHERIA YA MADAKTARI WA MIFUGO**

## 1. 0 Utangulizi

Tume ya Kurekebisha Tanzania ilianzishwa mwaka 1980, kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kufanya tafiti za sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia Tume pia inajukumu la kufanya tathmini za utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini kama malengo ya kuanzishwa kwa sheria hizo yanafikiwa.

Aidha Tume vilevile ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma ili kuweza kuwajengea wananchi uelewa wa sheria mbalimbali na hivyo kusaidia wananchi kushiriki katika maboresho ya sheria.

## 2.0 Sheria ya Madaktari wa Mifugo

Sheria hii imeanzisha Baraza la Madaktari wa Mifugo Tanzania. Baraza hili lina majukumu yafuatayo;

i. Kufanya usajili;

ii. Kusimamia utendaji wa madaktari wa mifugo, wasaidizi wa wataalam;

iii. Kumshauri na kupendekeza kwa Waziri mwenye dhamana na mifugo kuhusu masuala ya matibabu ya mifugo;

iv. Kusimamia utekelezaji wa matibabu ya mifugo;

v. Kutambua sifa, miundo mbinu kwa ajili ya mafunzo, taasisi na vyuo vya mafunzo;

vi. Kushirikiana na taasisi nyingine katika kupitisha mitaala ya mafunzo kwa ajili ya madakatri wa mifugo;

vii. Kuweka viwango vya chini katika – utekelezaji wa matibabu ya mifugo, kuchukua hatua za kinidhamu kuhusu mienendo ya utekelezaji wa matibabu;

viii. Kukuza mafunzo ya utaalam wa mifugo;

ix. Kutoa habari na elimu kuhusu utaalam wa matibabu ya mifugo.

**Baraza la madaktari wa mifugo linaongozwa na Msajili ambaye anajukumu la kutunza;**

i. Rejista ya wataalam wa mifugo;

ii. Sehemu za kutolea huduma za matibabu ya mifugo; na

iii. Orodha ya wataalam wa mifugo wasaidizi.

Sheria ya Madaktari ya Mifugo inaisha kuwa Baraza la Madaktari wa Mifugo litateua katika kila wilaya Msajili Msaidizi ambaye atatekeleza majukumu atakayokasimiwa na Msajili.

- **Wakaguzi**

Waziri mwenye dhamana na mifugo amepewa mamlaka ya kuteua wakaguzi kutoka katika wataalam waliosajiliwa. Wakaguzi hao wana majukumu yafuatayo:-

i. Kukagua miundombinu ya shughuli za kivetenari katika eneo la wilaya yake;

ii. Kupitia na kukagua vyeti vya usajili, leseni na vitabu;

iii. Kutoa ushauri kwa wakazi au waendesha miundombinu kuhusu usimamizi wa miundombinu ya kivetenari;

iv. Kuandaa taarifa za ukaguzi na kuziwasilisha katika Baraza la Vetenari Tanzania;

v. Kukamata madawa, vifaa, rekodi kama ushahidi wa makosa na;

vi. Kuchunguza masuala kuhusu magonjwa ya wanyama au afya ya wanyama katika eneo katika wilaya yake.

## 3.0 Usajili

Baraza litamsajili mtaalam wa vetenari kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake ikiwa;

i. Kwa daktari wa mifugo awe na shahada inayotambuliwa na Baraza la Madaktari wa Mifugo;

ii. Kwa daktari wa mifugo wabobezi.

**Sheria imeanisha watu ambao hawana sifa ya kusajiliwa. Watu hao ni;**

i. Muombaji ambaye amekutwa na hatia ya kosa la uwezo au uadilifu wake katika utekelezaji wa majukumu yake;

ii. Kwa maoni ya Baraza kuwa muombaji hastahili kusajiliwa kwa kuwa muombaji huyo ana matatizo ya akili ambayo yanaathiri utendaji kazi wake;

iii. Baraza litathibitisha kuwa shahada ya muombaji au nyaraka zilizowasilishwa kwa ajili ya usajili zilipatikana kwa njia ya udanganyifu; au

iv. Sifa ambazo muombaji ametumia kuombea zimeondolewa na Baraza la Madaktari wa Mifugo.

## 4.0 Utaratibu wa Uombaji Usajili

Mtu yeyote anaamua kuomba usajili anatakiwa kuomba kwa Msajili. Maombi hayo yanatakiwa kuambatana na vyeti vya elimu vilivyothibitishwa vya muombaji na ada ya usajili. Msajili atapeleka maombi hayo pamoja na mapendekezo yake kuhusu maombi hayo kwa Baraza wa ajili ya uamuzi. Baraza linaweza kukubali maombi hayo na Msajili atamsajili muhusika. Baraza pia linaweza kukataa maombi hayo na kumuelekeza Msajili kumjulisha muombaji na kueleza sababu za kukataa.

Mtaalam anayesajiliwa kama mtaalam wa vetenari au mtaalam mbobezi wa vetenari anaruhusiwa kutumia jina hilo la kitaalam kama linayoonyeshwa katika cheti cha usajili na kutekeleza utaalam wa vetenari.

Mtaalam wa nje ya Tanzania au Mtanzania ambaye ana sifa ya kuwa daktari wa mifugo au mbobezi anatakiwa kulipa ada na kufanya mtihani kabla ya kusajiliwa na Baraza.

## 5.0 Hitimisho

Sekta ya mifugo ni miongoni mwa sekta muhimu katika maendeleo ya nchi. Kutoka na umuhimu huo Sheria ya Madaktari wa Mifugo inalenga katika kutoa maekezo muhimu katika usimamizi wa majukumu ya taaluma ya madaktari wa mifugo.

---

**Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuwani ifuatayo:**

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na.1
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA - TANZANIA

tumesheria.tanzania | www.lrct.go.tz
@tumesheria | TumesheriaTv

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



## SHERIA YA MADAKTARI WA MIFUGO